© Manhaj ya Salafi e-Books 2002. www.manhajyasalafi.com

## Usool Ya pili

Ni Kuwa na maarifa ya dini ya **Kislamu** kwa ushahidi. Nayo ni **kujisalimisha** nafsi yako kwa Allaah na Tawheed na kunyenyekea katika kutii amri zake, pamoja na kujiepusha na shirk na watu wa shirk.

Na (usool ya pili) imegawanyika mafungu matatu; nayo ni **Al-Islaam, Imaan,** na **Ihsaan** - na kila fungu lina (arkaan) **nguzo** zake.

(Fungu la Kwanza) (arkaan) - Nguzo za Uislamu ni tano, nazo ni; *shahadatun an la ilaha ila Allaah wa ana Muhamadan rasulu Allaah* - ni kushudia kwamba hakuna Mola apasaye kuabudiwa kwa hakki ila Allaah na Muhammad ni Mtume wa Allaah, na kusimamisha sala, kulipa (kutowa) zakat, kufunga (mwezi wa) Ramadhaan na kwenda Hijja kwenye nyumba tukufu ya Allaah.

Na ushahidi wa **shahada** ni kauli ya Allaah (ta'la**):**

شَهِدَ ٱللَّهُ أَنَّهُۥ لَآ إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ وَٱلْمَلَٰٓئِكَةُ وَأُو۟لُوا۟ ٱلْعِلْمِ قَآئِمًۢا بِٱلْقِسْطِ ۚ لَآ
إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ ٱلْعَزِيزُ ٱلْحَكِيمُ ﴿١٨﴾

**Allaah ameshuhudia kwamba hakuna anaye stahili kuabudiwa kwa haki ila Yeye tu; na Malaika, na wenye ilimu (wote wame shuhudia hayo), (Allaah) ndiye Mwenye kusimamisha uadilifu; hapana apasaye kuabudiwa ila Yeye Mwenye Nguvu na Mwenye Hikima** (Soorah al-Imran 3:18)

Maana yake (*shahadatu an la ilaha ila Allaah*) ni **hakuna apasaye kuabudiwa kwa haki ila Allaah**:
- (la ilaha) ni kujiespusha na kuabudu chochote kando (asiekuwa) ya Allaah.
- (ila Allaah) kuthibitisha Ibadah kwa Allaah peke yake bila ya kumshirikisha, kama vile hakuna yeyote ambaye ana ushirika na Allaah kwenye kuumiliki Ulimwengu.

© Manhaj ya Salafi e-Books 2002. www.manhajyasalafi.com

Na tafsiri inayo dhihirisha hii (shahada) ni kauli ya Allaah (ta'la):

وَإِذْ قَالَ إِبْرَٰهِيمُ لِأَبِيهِ وَقَوْمِهِۦٓ إِنَّنِى بَرَآءٌ مِّمَّا تَعْبُدُونَ ﴿٢٦﴾
إِلَّا ٱلَّذِى فَطَرَنِى فَإِنَّهُۥ سَيَهْدِينِ ﴿٢٧﴾ وَجَعَلَهَا كَلِمَةًۢ بَاقِيَةً فِى عَقِبِهِۦ
لَعَلَّهُمْ يَرْجِعُونَ ﴿٢٨﴾

**Na (kumbuka) Ibrahim alipo mwambia baba yake na kaumu yake: Hakika mimi ninajitenga mbali na hayo munayo yaabudu, Isipo kuwa yule aliye niumba, kwani Yeye ataniongoa. Na akalifanya hili [**neno *laa ilaha ila llah*] **liwe neno lenye kubaki katika vizazi vyake ili warejee.** (Soorah az-Zukhruf 43: 26-28)

Na kauli ya Allaah (ta'la):

قُلْ يَٰٓأَهْلَ ٱلْكِتَٰبِ تَعَالَوْا۟ إِلَىٰ كَلِمَةٍ سَوَآءٍۭ بَيْنَنَا وَبَيْنَكُمْ أَلَّا نَعْبُدَ إِلَّا ٱللَّهَ
وَلَا نُشْرِكَ بِهِۦ شَيْـًٔا وَلَا يَتَّخِذَ بَعْضُنَا بَعْضًا أَرْبَابًا مِّن دُونِ ٱللَّهِ ۚ فَإِن تَوَلَّوْا۟
فَقُولُوا۟ ٱشْهَدُوا۟ بِأَنَّا مُسْلِمُونَ ﴿٦٤﴾

**Sema: Enyi Watu wa Kitabu! (mayahudi na manasara) Njooni kwenye neno lilio sawa baina yetu Na nyinyi: Ya kwamba tusimuabudu yeyote ila Allaah, wala tusimshirikishe na chochote; wala tusifanyane sisi kwa sisi kuwa waungu badala ya Allaah (au pamoja na Allaah). Na wakigeuka basi semeni: Shuhudieni ya kwamba sisi ni Waislamu.** (Soorah al-Imran 3:64)

Ushahidi kwamba Muhammad ni Mtume wa Allaah ni kauli ya Allaah (ta'la):

لَقَدْ جَآءَكُمْ رَسُولٌ مِّنْ أَنفُسِكُمْ عَزِيزٌ عَلَيْهِ مَا عَنِتُّمْ حَرِيصٌ عَلَيْكُم
بِٱلْمُؤْمِنِينَ رَءُوفٌ رَّحِيمٌ ﴿١٢٨﴾

**Hakika amekwisha kujieni Mtume kutokana na nyinyi wenyewe; yanamhuzunisha yanayo kutaabisheni; anakuhangaikieni sana. Kwa Waumini ni mpole na mwenye huruma**. (Soorah at-Tawba 9:128)

© Manhaj ya Salafi e-Books 2002. www.manhajyasalafi.com

Na maana ya *Muhamadan rasulu Allaah* (Muhammad ni Mtume wa Allaah) ni kumtii kwenye yale aliyo amrisha, kumuamini kwenye yale aliyo eleza, kujiepusha na yale aliyo kataza, na kumuabudu Allaah kwa yale aliyo amuru Mtume ﷺ (kwa mafundisho ya Mtume bila kuzidisha wala kupunguza).

Ushahidi wa salah na zakat na tafsiri ya Tawheed ni kauli ya Allaah (ta'ala)

وَمَآ أُمِرُوٓاْ إِلَّا لِيَعۡبُدُواْ ٱللَّهَ مُخۡلِصِينَ لَهُ ٱلدِّينَ حُنَفَآءَ وَيُقِيمُواْ ٱلصَّلَوٰةَ
وَيُؤۡتُواْ ٱلزَّكَوٰةَۚ وَذَٰلِكَ دِينُ ٱلۡقَيِّمَةِ ٥

**Nao hawakuamrishwa kitu ila wamuabudu Allaah kwa kumtakasia Dini, wawe waongofu, na wasimamishe Sala, na watoe Zakat. Na hio ndio Dini (ilio) madhubuti.** (Soorah al-Bayyinah 98:5)

Ushahidi wa kufunga (siyam) ni kauli ya Allaah (ta'la)

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ كُتِبَ عَلَيۡكُمُ ٱلصِّيَامُ كَمَا كُتِبَ عَلَى ٱلَّذِينَ مِن
قَبۡلِكُمۡ لَعَلَّكُمۡ تَتَّقُونَ ١٨٣

**Enyi mlio amini! Mmeandikiwa Saumu, kama walivyo andikiwa walio kuwa kabla yenu ili mpate kuchamngu** (Soorah al-Baqarah 2:183)

Ushahidi wa kuhijji (Hajj) ni kauli ya Allaah (ta'la)

وَلِلَّهِ عَلَى ٱلنَّاسِ حِجُّ ٱلۡبَيۡتِ مَنِ ٱسۡتَطَاعَ إِلَيۡهِ سَبِيلٗاۚ
وَمَن كَفَرَ فَإِنَّ ٱللَّهَ غَنِيٌّ عَنِ ٱلۡعَٰلَمِينَ ٩٧

**Na kwa ajili ya Allaah imewajibikia watu wahiji kwenye Nyumba hiyo, kwa yule awezae njia ya kwendea. Na atakaye kanusha basi Allaah si mhitaji kwa walimwengu.** (Soorah al-Imran 3:97)

(Fungo la pili) **Imaan** ina vitawi vya witiri sabini; ya juu kabisa ni kauli (*la ilaha ila Allaah*) hakuna apasaye kuabudiwa kwa haki ila Allaah, na ya chini kabisa ni kuondowa kitu cha kudhuru kwenye njia (tarika), na *al-hayaa* ni kitawi cha Imaan.

© Manhaj ya Salafi e-Books 2002. www.manhajyasalafi.com

Nguzo zake (Imaan) ni sita, nazo ni; kumwamini Allaah, na mailaka Wake, na vitabu Vyake , na Mitume wake, na siku ya mwisho, na kuamini *al-qadr* (kipimo) uzuri na ubaya wake.

Ushahidi wa hizi nguzo sita ni kauli ya Allaah (ta'ala)

لَّيْسَ ٱلْبِرَّ أَن تُوَلُّوا۟ وُجُوهَكُمْ قِبَلَ ٱلْمَشْرِقِ وَٱلْمَغْرِبِ وَلَٰكِنَّ ٱلْبِرَّ
مَنْ ءَامَنَ بِٱللَّهِ وَٱلْيَوْمِ ٱلْءَاخِرِ وَٱلْمَلَٰٓئِكَةِ وَٱلْكِتَٰبِ وَٱلنَّبِيِّۦنَ

**Sio wema kuwa mnaelekeza nyuso zenu upande wa mashariki na magharibi. Bali wema ni wa anaye muamini Allaah na Siku ya Mwisho na Malaika na Kitabu na Manabii** (Soorah al-Baqarah 2:177)

Ushahidi wa *al-qadr* ni kauli ya Allaah (ta'ala)

إِنَّا كُلَّ شَىْءٍ خَلَقْنَٰهُ بِقَدَرٍ ﴿٤٩﴾

**Kwa hakika Sisi tumekiumba kila kitu kwa (qadr) kipimo** (Soorah al-Qamar 54:49).

(Fungo la tatu) **Ihsaan** ni nguzo moja, nayo ni kumuabudu Allaah kana kwamba unamwona na hata kama humwoni basi (jua kuwa) yeye kwa hakika ana kuona. Ushahidi ni kauli ya Allaah (ta'ala)

إِنَّ ٱللَّهَ مَعَ ٱلَّذِينَ ٱتَّقَوا۟ وَّٱلَّذِينَ هُم مُّحْسِنُونَ ﴿١٢٨﴾

**Hakika Allaah yu pamoja na wenye kumcha, na watendao mema** (Soorah an-Nahl 16:128)

Na kauli ya Allaah ta'ala

وَتَوَكَّلْ عَلَى ٱلْعَزِيزِ ٱلرَّحِيمِ ﴿٢١٧﴾ ٱلَّذِى يَرَىٰكَ حِينَ تَقُومُ ﴿٢١٨﴾
وَتَقَلُّبَكَ فِى ٱلسَّٰجِدِينَ ﴿٢١٩﴾ إِنَّهُۥ هُوَ ٱلسَّمِيعُ ٱلْعَلِيمُ ﴿٢٢٠﴾

**Na umtegemee (Mola wako) Mwenye Nguvu Mwenye Kurehemu. Ambaye anakuona unapo simama, na mageuko yako kati ya wanao sujudu. Hakika Yeye ndiye Mwenye kusikia - Mwenye Kujua.** (Soorah ash-Shu'ara' 26:217-220)

© Manhaj ya Salafi e-Books 2002. www.manhajyasalafi.com

Na kauli yake

وَمَا تَكُونُ فِى شَأْنٍ وَمَا تَتْلُواْ مِنْهُ مِن قُرْءَانٍ وَلَا تَعْمَلُونَ مِنْ عَمَلٍ إِلَّا كُنَّا عَلَيْكُمْ شُهُودًا إِذْ تُفِيضُونَ فِيهِ

**Na huwi katika jambo lolote, wala husomi sehemu yoyote katika Qur'ani, wala hamtendi kitendo chochote ila Sisi huwa ni mashahidi juu yenu mnapo shughulika nayo** (Soorah Yoonus 10:61)

Ushahidi kutoka kwenye Sunnah ni hadithi iliyokuwa mashuri ya Jibreel *alaihi salaam* iliyopokelewa na 'Umar *radhiallahu anhu* aliyesema: Tulikuwa tumekaa kwenye hadhara ya Mtume (ﷺ) siku moja, alitujia mtu mwenye nguo nyeupe na nywele nyeusi sana. Hatukumwona na athari ya safari wala hakuna mmoja wetu anayemjua. Hata akakaa mbele ya Mtume (ﷺ) magoti yake yakaelekeana ma magoti ya Mtume (ﷺ) na akaweka mikono yake juu ya mapaja yake (ya mtume (ﷺ)). Na akasema: ya Muhammad nieleze kuhusu **Islaam.** Mtume (ﷺ) akasema: Uislamu ni; kushudia kwamba hakuna apasaye kuabudiwa kwa haki ila Allaah (*la ilaha ila Allaah*), na Muhammad ni Mtume wa Allaah, kusimamisha Salat, kulipa (kutowa) Zakat, kufunga (mwezi wa) Ramadhaan, na kwenda hijja kwenye nyumba (al-Kaabah) kwa yule mwenye uwezo. (Jibreel) Akasema: "umesema ukweli." Tukastaajabu kuwa ameuliza swali na halafu akasema kuwa umesema ukweli: (Jibreel) Akaendelea kusema: Nieleze kuhusu **Imaan.** (Mtume) akasema: Imaan ni kumwamini Allaah, na malaika wake, na vitabu vyake, na Mitume wake, na siku ya mwisho, na kuamini *al-qadr* uzuri na ubaya wake. (Jibreel) akasema: Umesema kweli. (Jibreel akaendelea) akasema: Nieleze kuhusu **Ihsaan.** (Mtume) akasema: ni kumuabudu Allaah kana kwamba unamwona na hata kama humwoni basi (jua ya kwamba) yeye kwa hakika ana kuona. (Jibreel) akasema: Nieleze kuhusu saa (ya mwisho). (Mtume) akasema: (hakika) anaye ulizwa hajui zaidi ya yule anaye uliza. (Jibreel) akasema: Basi nieleze kuhusu alama zake. (Mtume) akasema: Utaona watu walio na miguu mitupu wakiwa uchi, na wachungaji watule wakishindana kujenga nyumba ndefu za ghorofa. (Jibreel) Akaondoka, nasi tukabaki kwa muda kidogo. Mtume (ﷺ) akauliza: ya 'Umar (yaani ewe 'Umar), wamjua yule mwenye kuuliza maswali alikuwa ni nani? Nikajibu: "Allaah na Mtume wake wanajuwa bora zaidi". Akasema: alikuwa ni Jibreel, alikuja kuwafunzeni dini yenu.